VIASHIRIA VYA UTOAJI HUDUMA
Afya | Elimu

# TANZANIA
## Viashiria Vya Utoaji Huduma

ELIMU | MEI 2016

Tanzania imeonyesha maendeleo ya kuvutia katika sekta yake ya elimu katika kipindi cha takribani muongo mmoja uliyopita. Viwango vya kumaliza shule za msingi viliongezeka kutoka 55% mwaka 2000 hadi 80% mwaka 2012. Tanzania pia ilifanikisha usawa wa kijinsia kwa wanafunzi na walimu. Pamoja na maendeleo haya ambayo ni chanya sana, imeonekana kwamba sehemu kubwa ya wanafunzi wa Kitanzania hawajifunzi mashuleni. Matokeo haya yana uwezekano mkubwa kuwa na uhusiano na ubora duni wa utoaji huduma. Mfumo wa elimu wa Tanzania unahitajika sasa kutoa ubora kwa wanafunzi wake ili kuwapatia nyenzo za kukabiliana na ushindani katika masoko ya kazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

**Viashiria vya Utoaji Huduma katika Mnyororo wa Matokeo ya Elimu**

**Upatikanaji wa Vifaa**
- Miundombinu 41%
- Vifaa vya Mwalimu 61%
- Wanafunzi na Vitabu 25%
- Uwiano wa Mwanafunzi-Mwalimu 43:1

**Juhudi za Mwalimu**
- Utoro shuleni 14%
- Utoro darasani 47%

**Uwezo wa Mwalimu**
- Alama za Mtihani 59%
- Kiwango cha chini cha Maarifa 21%

**Jinsia**
- Walimu wa Kike Msingi 50%
- Walimu wa Wakuu wa Kike 18%

**Matokeo ya Kujifunza**
- Kiingereza 37%
- Kiswahili 81%
- Hesabu 58%

# Mambo Muhimu

### *Upatikanaji wa vifaa*

- Katika shule za msingi za Kitanzania, kuna upungufu mkubwa katika upatikanaji wa vifaa katika ngazi ya shule. Ni 41% tu ya shule ndizo zilizo na miundombinu inayokidhi kiwango cha chini cha mahitaji; 47% tuu zina vyoo vinavyokidhi viwango; na 61% pekee zina vifaa vya kufundishia vinavyokidhi kiwango cha chini cha mahitaji. Ndani ya darasa, ni mwanafunzi mmoja kati ya wanne (25%) ana kitabu cha kiada cha hesabu au Kiingereza. Uchunguzi wa darasani umeonyesha wastani wa uwiano wa mwanafunzi kwa mwalimu kuwa ni wanafunzi 43 kwa mwalimu mmoja, ambao ni chini kidogo ya kiwango kinachotarajiwa cha 45:1.

### *Juhudi za mwalimu*

- Kwa wastani, 14% ya walimu waligundulika kutokuwepo shuleni. Utoro kutoka darasani ulikuwa juu zaidi ambapo 37% ya walimu waliokuwepo shuleni, hawakuwepo darasani wakifundisha. Darasani, walimu walitumia takribani 12% ya muda kwenye shughuli ambazo si ufundishaji. Ukichanganya viashiria hivi vitatu, matokeo yanaonyesha kwamba wanafunzi wana masaa 2 na dakika 47 tu ya muda wa kufundishwa kila siku.

### *Uwezo wa mwalimu*

- Idadi kubwa ya walimu hawana stadi za kitaaluma na uelimishaji zinazohitajika ili kufundisha. Ijapokuwa alama za wastani wa ufaulu kwenye majaribio ya Kiingereza na hisabati ilikuwa 59%, 21% tu ya walimu walipata 80% au zaidi katika ufaulu wa majaribio haya.

### *Ufaulu wa mwanafunzi*

- Wanafunzi walipata alama za juu zaidi katika mtihani wa Kiswahili (65%) ukilinganisha na mtihani wa Kiingereza (50%). Wastani wa alama katika mtihani wa Kiingereza ulikuwa chini katika 37%, wakati, kwenye mtihani wa Kiswahili, wastani wa alama ulikuwa 81%. Cha kustaajabisha, alama za hesabu za wanafunzi zilifanana, ikiwa wastani wa 58%, bila ya kujali lugha iliyotumika.
- Mtihani wa hesabu umedhihirisha kwamba wanafunzi wengi hawakufanya vizuri katika ngazi ya darasa la 3. Kwa mfano, ni 40% ya wanafunzi wa darasa la 4 waliweza kufanya hesabu ya 6 ÷ 3 au 7 x 8.

### *Masuala ya Jinsia*

- Tanzania ilifanikisha usawa wa kijinsia katika nguvu kazi ya ualimu, hata hivyo, ni 18% ya wanawake ndio waliweza kufikia kiwangoi cha kuwa walimu wakuu. Hii inamaanisha kuwa, walimu wa kike wana uwezekano mdogo mara tano kuongoza shule ukilinganisha na wanaume. Shule zinazoongozwa na wanawake zina walimu wanawake 27% zaidi ya zile zinazoongozwa na wanaume. Upungufu huu wa kijinsia ulionekana zaidi katika shule za vijijini zinazoongozwa na wanaume, zilizokuwa na uwiano wa mwalimu wa kiume kwa wa kike kuwa 2:1.
- Ukichukulia uhusiano kati ya jinsia ya mwalimu na ufaulu wa mitihani wa mwanafunzi, matokeo yanaonesha kwamba wavulana walifanya vibaya zaidi katika hesabu wakiwa na mwalimu mwanamke. Hata hivyo, ufaulu wa mwalimu katika majaribio yote mawili ya Kiingereza na hesabu una matokeo chanya kwenye alama za ufaulu katika jaribio la hesabu kwa wasichana. Kadri walimu wanawake walivyo wengi katika shule, ndivyo kadri wasichana wanavyofanya vizuri kwenye Kiingereza, ijapokuwa ufaulu wa wavulana haukuonesha hayo mahusiano.

### *Mahusiano kati ya juhudi na utendaji wa mwalimu na matokeo ya kujifunza ya mwanafunzi*

- Kwa kila siku, walimu wa Kitanzania hufika shuleni, lakini mara wanapokuwa hapo, wengi hawakutumia muda mwingi darasani. Ukweli huu umewafanya wanafunzi wa Kitanzania kupoteza zaidi ya 50% ya muda uliopangwa wa kufundishwa, na hukutana na walimu kwa masaa 2 na dakika 47 tu kwa siku.

# Matokeo ya Viashiria vya Utoaji Huduma

## *Upatikanaji wa Vifaa Muhimu*


Kwa vigezo vya upatikanaji wa vifaa vya kufundishia, ni 61% tu ya shule za msingi za Tanzania ndio zinakidhi kwa kiwango cha chini cha mahitaji. Viashiria vyote vidogo vilikaribia 100% isipokuwa "mwanga wa kutosha kuweza kusoma ubao". Zaidi ya 25% ya vyumba vya madarasa vya darasa la 4, huwezi kuona vizuri maandishi ubaoni ukiwakatika kona ya mwisho wa darasa.

Karibu shule zote za msingi za Tanzania vyoo vilipatikana, na karibu vyote vilifikika na vilikuwa visafi[1]. Kutokana na ukweli kwamba shule nyingi (hasa katika maeneo ya vijijini), walimu hawakuwa na vyoo tofauti na wanafunzi, ilichukuliwa kwamba chini ya 57% ya shule ndizo zilikuwa na vyoo binafsi. Kwa wastani, ni 25% ya wanafunzi ndio wanaweza kupata kitabu cha Kiingereza au hesabu katika darasa la 4 la kawaida. Kwa 42% ya shule, hakuna mwanafunzi aliyekuwa na kitabu cha kiada wakati wa kipindi.

## *Juhudi za mwalimu: Je, watoa huduma wanafanya nini?*

Utoro shuleni kwa kiasi ulikuwa mdogo ambapo14% ya waalimu hawakuwepo shuleni wakati wa ziara ya kushtukiza. Hata hivyo, karibu 37% ya walimu waliokuwepo shuleni hawakuwepo darasani wakifundisha. Hii iliongeza kiwango cha utoro darasani hadi 47% kitaifa. Hivyo, kwa wakati wowote ule, takribani nusu ya walimu wa shule za Msingi nchini walikuwa nje ya chumba cha darasa wakiwa hawafundishi. Kwa vile matumizi kwa walimu huwakilisha sehemu kubwa zaidi ya matumizi ya sekta ya elimu nchini Tanzania, kiwango hiki cha juu cha utoro ni dhahiri kinafanya upotevu mkubwa wa muda na rasilimali. Kuna uwezekano mkubwa kwamba utoro wa darasani ni suala la uongozi wa shule na menejimenti, kwa sababu walimu wengi, kiukweli, walikuwepo shuleni.

**KIELELEZO 1.** **Sehemu walipo walimu wakati wa ziara ya kushtukiza (asilimia)**




**Wanafunzi wanapata wastani wa masaa 2 na dakika 46 za kufundishwa kila siku badala ya muda rasmi wa masaa 5 na dakika 56.**

Ili wanafunzi wajifunze, mwalimu anatakiwa awepo shuleni, ndani ya chumba cha darasa na akifundisha kwa dhati. Matokeo ya Viashiria vya Utoaji Huduma yanaonyesha kwamba 14% ya walimu hawakuwepo shuleni wakati wa ziara ya kushtukiza, inayomaanisha hasara ya dakika 51 ya muda wa kufundisha; na walimu wengine 37% walikuwepo shuleni, lakini sio ndani ya chumba cha darasa ambako walitakiwa kufundisha, iliyopelekea saa 1 na dakika 54 nyingine za muda wa kufundisha uliopotea. Wakiwa darasani, walimu walifundisha 88% ya muda, iliyosababisha upotevu wa dakika 23 za muda wa kufundisha. Ukilimbikiza vyanzo vya muda wa kufundisha uliopotea, wanafunzi walipata takribani 39% ya muda uliopangwa wa kufundishwa. Hii inamaanisha kwamba wanafunzi wanapata wastani wa masaa 2 na dakika 46 za kufundishwa kila siku badala ya muda rasmi wa masaa 5 na dakika 56.

## *Uwezo wa mwalimu: Je, watoa huduma wanajua nini?*

Uwezo wa maarifa miongoni mwa walimu wa Kitanzania uikuwa duni. Ni mwalimu 1 tu kati ya walimu 5 aliyepata alama zaidi ya 80% katika jaribio lililojumuisha Kiingereza na hesabu. Kitaifa, walimu wengi walionesha viwango vya chini vya uwezo wa maarifa, ambayo kimsingi ilitokana na matokeo mabaya katika somo la Kiingereza- ni 1.1% ya walimu walikuwa juu ya alama iliyowekwa ya 80%. Walimu wa hesabu walifanya vizuri zaidi kwa kuwa na mwalimu 1 kati ya 3 aliyepata 80% au zaidi katika mtihani.

Ukichukua Kiingereza na hesabu pamoja, walimu waliweza kujibu kwa usahihi 59% ya maswali. Walimu walifanya vibaya kwenye Kiingereza (42%), na katika ufundishaji (36%).

1 Tafadhali zingatia kwamba kwa kiashiria hiki shule nyingi hazikuwa na taarifa kuhusu usafi na kufikika kwa vyoo. Shule mahususi ambazo zilikosa taarifa zilikuwa ni zile ambazo walimu na wanafunzi wanatumia choo kimoja. Kwa shule kama hizo, swali hilo lilirukwa katika dodoso la lugha ya Kiswahili. Tulichukulia kwamba shule hizo hazikukidhi kigezo cha faragha kwa wanafunzi. Hata hivyo, vyoo vilichukuliwa kuwa vinafikika na ni safi. Hivyo, kigezo cha miundombinu kilitoa sifa za juu zaidi kuliko hali halisi ilivyo katika shule za msingi nchini Tanzania.


Ufaulu duni katika mtihani wa Kiingereza unaonyesha kwamba walimu hawajaelewa nusu ya mtaala wa darasa la 4. Walimu walipata ufaulu wa chini kabisa katika zoezi la insha (21%). Wanapopewa zoezi la kusahihisha barua yenye makosa 21, kama vile kuweka koma, au herufi kubwa au msamiati, mwalimu wa Kitanzania wa wastani wa shule ya msingi, aligundua makosa 4.6 tu kati ya hayo.

**Wanapopewa zoezi la kusahihisha barua yenye makosa 21, kama vile kuweka koma, au herufi kubwa au msamiati, mwalimu wa Kitanzania wa wastani wa shule ya msingi, aligundua makosa 4.6 tu kati ya hayo.**


Kwenye mtihani wa hesabu, wastani wa alama ulikuwa -63% pakiwa na tofauti kubwa na muhimu (pointi asilimia 19) baina ya alama kwenye sehemu ya chini na juu ya mtaala wa msingi. Hii ina maana kwamba walimu walikuwa na uwezo wa kufanya hesabu rahisi, kama vile kujumlisha namba zenye tarakimu mbili au tatu, kuliko hesabu ngumu kidogo, kama vile kulinganisha visehemu.

Kwenye sehemu ya ufundishaji, walimu waliweza kufanya theluthi moja tu ya maswali kwenye mtihani. Walimu wote walionekana kuwa na stadi duni za ufundishaji, ambayo ilionyeshwa wazi na kiashiria cha "kiwango cha chini cha maarifa", ambapo ni mwalimu 1 tu kati ya walimu 1000 (0.1%) ndiye aliyepata zaidi ya 80%. Matokeo haya yanamaanisha kwamba walimu wanajua kiasi kidogo tu zaidi ya wanafunzi wao, na kile wanachokijua, hawawezi kukifundisha vizuri.

**KIELELEZO 2. Wastani wa alama za walimu katika mtihani wa Kiingereza, hesabu, na ufundishaji (asilimia)**




**KIELELEZO 3. Ufaulu wa mwanafunzi – alama za wastani (asilimia)**




## *Ufaulu wa mwanafunzi*

Kama ilivyotarajiwa, wanafunzi walipata alama za juu zaidi katika jaribio la Kiswahili ukilinganisha na laKiingereza. Wanafunzi waliofanya jaribio laKiswahili walijibu kwa usahihi 65% ya maswali kwa ujumla ukilinganisha na 50% ya wale waliofanya jaribio la Kiingereza. Wastani wa ufaulu katika sehemu ya Kiingereza ilikuwa 37 tu, ukilinganisha na wastani wa 81% katika sehemu ya Kiswahili. Inaleta shauku kuona kwamba makundi yote mawili ya wanafunzi yanakuwa na alama sawa za wastani katika jaribio la hesabu (58%). Wanafunzi wa Dar es Salaam waliwazidi kwa kiasi kikubwa wanafunzi katika maeneo mengine yote ya nchi. Hata hivyo, wasichana na wavulana walikuwa na ufaulu unaofanana.

Kwa Kiswahili, takribani wanafunzi 9 kati ya 10 waliweza kufanya maswali rahisi sana, kama vile kutambua herufi au kutambua neno rahisi. Kwa kweli, waliofanya mtihani wa Kiswahili walifanya vizuri hata waliposoma aya ya maneno hamsini (75%). Hata hivyo, katika Kiingereza, wanafunzi walishindwa kutambua herufi rahisi za alfabeti mara 1 kati ya mara 4 walipotakiwa kufanya hivyo. Ukichukulia mazoezi magumu zaidi, mwanafunzi 1 kati ya wanafunzi 3 aliweza kusoma sentensi yenye maneno kumi, na 2.7% waliweza kusoma kwa ufasaha aya ya maneno-58 waliyopewa.

Katika hesabu, 60% ya wanafunzi waliweza kujumlisha namba 2 zilizo na tarakimu tatu, na 42% waliweza kutoa namba mbili zenye tarakimu mbili, lakini utendaji wao ulishuka hadi 18% katika kugawanya tarakimu mbili, na hadi 12% kwa hesabu za kuzidisha tarakimu mbili. Mtihani ulionyesha kwamba wanafunzi wengi wa darasa la 4 hawakufanya vizuri katika kiwango cha darasa la 3. Ni 40% tu ya wanafunzi wa darasa 4 waliweza kufanya hesabu ya 6 ÷ 3 au 7 x 8, ambayo

kwa kweli ni sehemu ya mtaala wa darasa la 3. Wanafunzi wa Dar es Salaam walifanya vizuri zaidi kwa ujumla, wakifuatiwa na wanafunzi katika maeneo mengine ya mijini, ambao nao pia walifanya vizuri zaidi ya wanafunzi wa vijijini.

## *Masuala ya Jinsia*

### Jinsia katika nguvu kazi ya ualimu

Tanzania imefanikiwa katika kufanikisha usawa wa kijinsia kwa walimu katika mfumo wake wa elimu ya msingi. Wanawake ni 50% ya idadi ya walimu wote wa shule za msingi. Dar es Salaam 84% ya walimu wote ni wanawake, wakati katika maeneo mengine ya mijini wanawake ni 74% ya walimu. Tofauti ni kwamba, ni 40% tu ya walimu ni wanawake katika shule za vijijini.

**Tanzania imefanikiwa katika kufanikisha usawa wa kijinsia kwa walimu katika mfumo wake wa elimu ya msingi.**

Hata hivyo, katika menejimenti za shule, wanawake walikuwa na uwakilishi mdogo sana, ambapo 18% tu ya walimu wakuu ni wanawake. Wanawake walikuwa na uwezekano mdogo mara 5 kuongoza shule ukilinganisha na wanaume, ijapokuwa walikuwa na uwakilishi sawa katika nguvu kazi ya ualimu. Maeneo ya vijijini yalionyesha upungufu mkubwa wa walimu wakuu wa kike (14%), lakini ilikuwa katika jiji la Dar es Salaam ndiko ambako pengo la kijinsia (38%) lilikuwa kubwa zaidi.

Shule zilizoongozwa na wanawake zilikuwa na wastani wa 27% ya walimu wa kike zaidi, tofauti ambayo ni kubwa na stahiki. Kwa wastani, walimu 7 kati ya 10 walikuwa wanawake katika shule zinazoendeshwa na mwanamke, ukilinganisha na walimu wa kike zaidi kidogo ya 4 kati ya 10 katika shule zinazoongozwa na wanaume. Ni ukweli, kwamba wanawake ndio wengi katika nguvu kazi ya ualimu katika shule zote, isipokuwa katika shule za vijijini zinazoongozwa na wanaume, ambako kulikuwa na uwiano wa mwalimu wa kiume kwa wa kike wa 2:1.

## *Jinsia ya Mwalimu na Matokeo ya Mwanafunzi*

Takwimu zinaonesha jinsi gani jinsia ya mwalimu ina athari kwa watokeo ya mtihani ya mwanafunzi. Matokeo yanaonesha kwamba kuwepo na mwalimu wa kike kuna athari hasi katika alama za mwanafunzi kwenye hesabu, na kwa kiwango kikubwa kwenye ufaulu wa wavulana, ikimaanisha kwamba wavulana walifanya vizuri zaidi katika hesabu wakiwa na mwalimu wa kiume, lakini kwa wasichana haikuleta tofauti. Hata hivyo, ufaulu wa mwalimu katika majaribio yote mawili yaani la Kiingereza na hesabu ulikuwa na athari chanya na stahiki katika alama za hesabu za wasichana (kwa maana, kadri alama za mwalimu zinavyokuwa juu, ndivyo kadri ufaulu wa hesabu wa wasichana unavyokuwa mzuri). Mwisho, kadri walimu wa kike walivyo wengi katika shule, ndivyo wasichana wanavyofanya vizuri zaidi katika Kiingereza, lakini mahusiano haya hayakuonesha tofauti ufaulu wa wavulana.

## *Uhusiano kati ya juhudi na utendaji wa mwalimu na matokeo ya kujifunza ya mwanafunzi*

Walimu wengi wa Kitanzania wanahudhuria shuleni kila siku, lakini mara wanapokuwa hapo, wengi wao hawatumii muda mwingi darasani kufundisha wanafunzi wao. Kwa kiwango kikubwa, wanafunzi walikuwa peke yao darasani ilihali mwalimu alikuwa anajihusisha na shughuli zisizohusiana na kufundisha. Kutokana na ukweli huu, wanafunzi wa Kitanzania walipoteza zaidi ya nusu ya muda wa kufundishwa waliotakiwa kuupata na waliweza kukutana na walimu wao kwa masaa 2 na dakika 46 tu kwa siku, badala ya muda unaotakiwa yaani masaa 5 na dakika 56. Matokeo pia yanaashiria kwamba ufaulu wa wanafunzi unaweza kuongezeka kadri uwezo wa mwalimu katika hesabu unavyoongezeka, au iwapo msongamani wa wanafunzi katika darasa utapunguzwa kwa kiasi kikubwa.

## *Je, Tanzania inalingana vipi na nchi nyingine za Viashiria vya Utoaji Huduma?*


Kwa viashiria vilivyozoeleka vya ubora, kama vile vifaa au miundombinu, Tanzania ilikuwa inafanya vibaya ukilinganisha na majirani zake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ni 61% tu ya shule za Tanzania zilikuwa na rasilimali za kufundishia zinazokidhi kiwango cha chini kinachokubalika ukilinganisha na 81% kwa Uganda na 79% kwa Kenya katika kiashiria hicho. Hata hivyo, shule za Tanzania zilifanya vizuri zaidi katika rasilimali za kufundishia kuliko Nigeria (48%) au Togo (24%). Wanafunzi wa Kitanzania walikuwa na uwezekano mkubwa mara 4 zaidi kutumia kitabu cha kiada darasani kuliko wenzao wa Uganda. Kinyume chake, wanafunzi wa nchini Togo na Nigeria walikuwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kutumia kitabu cha kiada darasani, Togo wakiwa na 76% na Nigeria 34% ya wanafunzi. Linapokuja suala la juhudi za walimu, Tanzania na Kenya zilionyesha utoro mdogo katika kufika shuleni, lakini utoro wa hali ya juu katika kuhudhuria darasani, ambapotakribani nusu ya walimu hawapo darasani wakati wowote ule. Uganda ilikuwa na utoro wa hali ya juu zaidi kwa vigezo vyote viwili, yaani, utoro mashuleni na utoro madarasani. Walimu wa Kitanzania pamoja na wenzao wa Kenya (wanaofanya vizuri

zaidi) na Uganda, ambazo ni majirani, walifanya vizuri zaidi kwa kiwango kikubwa kuliko walimu wa Nigeria na Togo katika maarifa. Walimu wa Kitanzania walikuwa wa mwisho katika stadi za lugha miongoni mwa hizo nchi tano. Katika hesabu, Walimu wa Kitanzania walikuwa wa pili, nyuma ya wale wa Kenya, japokuwa waliweza kupata alama nzuri zaidi katika kulinganisha visehemu, ambapo pia walipata alama mara mbili zaidi ya walimu wa Uganda. Katika ufundishaji, walimu wa Kitanzania walikuwa sawa na wa Kenya lakini walliwazidi wa Uganda. Walikuwa mara mbili ya alama za walimu wa Afrika Magharibi. Walimu nchini Tanzania waliwazidi wengine wote katika "kutayarisha mpango wa somo," lakini hawakufanya vizuri katika stadi za "kupima uwezo wa watoto".


## Kuilinganisha Tanzania kwa vipindi tofauti

Tanzania, pamoja na Senegal, zilianzisha programu ya Viashiria vya Utoaji Huduma (SDI) mwaka 2010. Kwa sehemu kubwa, hili limewezesha kulinganisha mienendo katika utoaji huduma kati ya mwaka 2010 na 2014. Kwa kigezo cha upatikanaji wa miundombinu ya msingi, hapakuwepo na maboresho makubwa katika miaka minne tangu kuanza kwa programu ya kwanza ya SDI. Ni 2% tu ya shule ndio zina umeme, maji safi, usafi wa vyoo na mazingira yaliyoboreshwa katika mwaka 2014, kiwango ambacho ni chini ukilinganisha na 3% ambacho kilikuwa ni kiwango cha mwaka 2010. Idadi ya wanafunzi katika darasa la 4 ilipungua sana kutoka wanafunzi 52 hadi 43, punguzo la takribani 20%. Palikuwepo na maendeleo makubwa katika utoro shuleni, ambao ulipungua kutoka 23% mwaka 2010 hadi 14% mwaka 2014, ambalo ni punguzo la 40%. Hata hivyo, ijapokuwa utoro wa darasani ulipungua kutoka 53% hadi 47%, kupungua huku hakukuwa na maana sana kitakwimu, ikimaanisha kwamba takribani nusu ya walimu walikuwa bado hawako darasani. Kupungua kwa utoro wa walimu kuliwanufaisha wanafunzi ambao, kati ya mwaka 2010 na 2014, ziliongezekadakika 43 za muda wa kufundishwa kwa siku. Katika mwaka wa kawaida wa shule (wenye wastani wa siku 194), hili lilikuwa ongezeko la siku 24 kamili za kufundisha. Cha kuvutia zaidi, wanafunzi wa mijini waliongeza mara dufu muda wa kuwa na walimu kutoka siku 47 mwaka 2010 hadi siku 94 mwaka 2014. Hata hivyo, ni vizuri kukumbuka kuwa wanafunzi wa shule za msingi wa Tanzania bado wanapoteza zaidi ya nusu ya muda wao uliopangwa wa kufundishwa. Kiwango cha chini kinachokubalika cha walimu cha maarifa ya somo hakikuonyesha maboresho kati ya 2010 na 2014, wakati utendaji wa walimu katika somo la Kiingereza ukiendelea kuwa mbaya Zaidi katika kipindi hiki. Ufaulu wa wanafunzi katika majaribio uliongezeka katika baadhi ya maeneo. Ijapokuwa ufaulu katika Kiingereza ulibaki kuwa duni ukiwa na wastani wa alama takribani 40%, alama za jumla za wanafunzi katika hesabu ziliongezeka kwa kiwango kikubwa kutoka 39% hadi 58% katika kipindi cha miaka hii minne .


**KIELELEZO 4. Mgawanyo wa walimu wa kike katika shule kwa cheo**




**KIELELEZO 5. Mgawanyo wa walimu wa kike katika shule kulingana na jinsi ya mwalimu mkuu**




**KIELELEZO 6. Kuanzia muda uliopangwa rasmi hadi muda halisi wa kufundisha**



## Je, hii ina maana gani kwa Tanzania?

Kwa kutambua umuhimu wa elimu katika maendeleo ya kiuchumi, Tanzania imeongeza uwekezaji wake katika sekta ya elimu katika kipindi cha miaka 10 iliyopita. Nchi ilipata mafanikio katika uwekezaji huu kwani kiwango cha kumaliza shule ya msingi kiliongezeka kutoka 55% mwaka 2000 hadi zaidi ya 80% mwaka 2012. Usawa wa kijinsia pia umefanikishwa katika elimu ya msingi na wasichana wanawakaribia wavulana kwa kasi katika sekondari. Hata hivyo, janga la hivi karibuni la mwaka 2012 la matokeo ya kidato cha 4 ulikuwa ni uamsho kwa Serikali ya Tanzania na wadau wote wa elimu kwamba zaidi ya viashiria vya upatikanaji, ubora wa elimu ni kipengele muhimu sana ambacho hakipaswi kupuuzwa.

Matokeo ya mwaka 2014 ya Viashiria vya Utoaji Huduma (SDI) yanaonesha kwamba Tanzania kwa wastani inafanya vizuri katika kigezo cha viwango vya utoro wa walimu shuleni. Hata hivyo, walimu wanahitaji kusimamiwa vizuri zaidi, kwa sababu kuwakuta walimu shuleni haimaanishi kwamba watakuwa darasani wakifundisha. SDI pia inaonyesha kwamba shule za msingi za Tanzania zinahitaji maboresho kwa maana ya miundombinu na vifaa vya kufundishia.

Wakati ni mwalimu mmoja tu kati ya watano ndiye anayemudu mtaala wa kufundisha, uwezo wa walimu (au kukosa uwezo) wa kufundisha somo ni jambo muhimu na linahitaji kushughulikiwa. Ukosefu wa stadi za ufundishaji ni suala la haraka zaidi, ambapo ni mwalimu 1 tu katika 1000 aliyepata alama zaidi ya 80% zinazohitajika. Kuna ushahidi wa kutosha kwamba maarifa ya walimu na uwezo wao wa kuuhamisha kwenda kwa wanafunzi (kwa maana ya stadi za ufundishaji) ni kichocheo cha matokeo ya kujifunza ya mwanafunzi.

Sasa ni muda muafaka wa kuwekeza katika ubora wa elimu na serikali imeanza mchakato huu kupitia mpango wa 'Matokeo Makubwa Sasa' ambao unatambua wazi kwamba ubora ndio eneo jipya na njia erevu ya kuboresha matumizi ya umma katika elimu kwa kuzingatia 'thamani ya fedha'.

# Jicho la Haraka

**JEDWALI 1. Kulinganisha matokeo ya SDI kwa Eneo la Kijiografia**

| Viashiria | TANZANIA | Dar es Salaam | Niji Mingine | Vijijini | EQUIP-T | Vijiji Vyote | Miji Yote |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ***Wanachofanya watoa huduma (juhudi)*** | | | | | | | |
| Kiwango cha utoro wa shule (% ya walimu) | 14.4 | 17.8 | 13.7 | 14.3 | 8.3 | 14.3 | 14.6 |
| Kiwango cha utoro wa darasani (% ya walimu) | 46.7 | 42.9 | 46.7 | 47.0 | 43.5 | 47.0 | 45.8 |
| Muda wa kufundisha darasani (Muda wa Kazi) | saa 2 dak 46 | saa 2 dak 42 | saa 2 dak 43 | saa 2 dak 47 | saa 2 dak 32 | saa 2 dak 47 | saa 2 dak 42 |
| | saa 5 dak 56 | saa 5 dak 41 | saa 5 dak 50 | saa 5 dak 57 | saa 5 dak 58 | saa 5 dak 57 | saa 5 dak 48 |
| ***Wanachojua watoa huduma (uwezo)*** | | | | | | | |
| Maarifa ya chini ya mwalimu | 21.5 | 26.2 | 22.3 | 21.0 | 19.5 | 21.0 | 23.2 |
| ***Wanachoweza kufanyia kazi watoa huduma (upatikanaji wa rasilimali)*** | | | | | | | |
| Uwiano wa mwanafunzi – mwalimu ulioonekana | 43.5 | 69.8 | 58.9 | 40.7 | 46.1 | 40.8 | 60.4 |
| Mgawanyo wa wanafunzi wenye vitabu vya kiada (%) | 25.3 | 31.0 | 14.1 | 26.7 | 22.2 | 26.7 | 16.7 |
| Kiwango cha chini cha upatikanaji wa vifaa (%) | 61.4 | 83.2 | 80.1 | 58.3 | 58.9 | 58.3 | 80.4 |
| Kiwango cha chini cha upatikanaji wa miundombinu (%) | 40.4 | 67.0 | 61.4 | 36.8 | 34.3 | 36.9 | 62.3 |
| Upatikanaji wa miundombinu | 2.3 | 15.7 | 9.6 | 0.8 | 0.0 | 0.9 | 10.2 |

Maelezo: (a) Ukilinganisha na SDI 2010 (kwa maana shule ina umeme, choo na maji safi). Chanzo: Tanzania SDI 2014 na takwimu za mtunzi.

**JEDWALI 2. Mlinganisho wa matokeo ya Viashiria vya Utoaji Huduma (SDI) katika nchi mbalimbali (shule za umma tu)**

| | Tanzania* 2014 | Wastani wa SDI | Kenya 2012 | Msumbiji+ | Nigeria** | Senegal | Tanzania+ 2010 | Togo | Uganda |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ***Wanachojua watoa huduma (uwezo wa mwalimu)*** | | | | | | | | | |
| Kiwango cha chini cha maarifa | 22 | 15 | 40 | 0 | 4 | Haiwezi Kulinganishwa | Haiwezi Kulinganishwa | 2 | 12 |
| (sio chini ya 80% katika lugha na hesabu) | 48 | 43 | 57 | 27 | 33 | Haiwezi Kulinganishwa | Haiwezi Kulinganishwa | 36 | 43 |
| ***Wanachofanya watoa huduma (juhudi za mwalimu)*** | | | | | | | | | |
| Kiwango cha utoro wa shule | 14 | 19 | 14 | 45 | 14 | 18 | 23 | 21 | 26 |
| Kiwango cha utoro wa darasani | 47 | 40 | 42 | 56 | 19 | 29 | 53 | 36 | 52.8 |
| Muda rasmi uliopangwa wa kufundisha | saa 5 dak 55 | saa 5 dak 34 | saa 5 dak 37 | saa 4 dak 17 | saa 5 dak 53 | saa 4 dak 36 | saa 5 dak 12 | saa 5 dak 29 | saa 7 dak 18 |
| Muda unaotumika kufundisha kwa siku | saa 2 dak 47 | saa 3 dak 02 | saa 2 dak 49 | saa 1 dak 41 | saa 3 dak 26 | saa 3 dak 15 | saa 2 dak 04 | saa 3 dak 29 | saa 3 dak 18 |
| ***Walichonacho watoa huduma (upatikanaji wa rasilimali)*** | | | | | | | | | |
| Uwiano wa mwanafunzi – mwalimu ulioonekana | 44 | 40 | 35 | 21 | 22 | 27 | 52 | 29.7 | 48 |
| Mgawanyo wa wanafunzi wenye vitabu vya kiada | 25 | 37 | 48 | 68 | 38 | 18 | 20 | 69 | 5 |
| Kiwango cha chini cha vifaa vinavyopatikana | 61 | 61 | 79 | 77 | 55 | Haiwezi Kulinganishwa | Haiwezi Kulinganishwa | 27 | 81 |
| (90% na penseli na daftari) | 40 | 38 | 60 | 29 | 19 | Haiwezi Kulinganishwa | Haiwezi Kulinganishwa | 22 | 54 |
| ***Kiwango cha chini cha upatikanaji wa miundombinu*** | | | | | | | | | |
| Alama ya mtihani (kati ya 100) (lugha, hesabu) | 40+* | 50 | 72 | 21 | 32 | Haiwezi Kulinganishwa | Haiwezi Kulinganishwa | 46 | 49 |
| Alama ya mtihani wa Lugha | 37+* | 50 | 76 | 19 | 31 | Haiwezi Kulinganishwa | Haiwezi Kulinganishwa | 46 | 47 |
| Alama ya mtihani wa Hesabu | 58 | 47 | 59 | 25 | 32 | Haiwezi Kulinganishwa | Haiwezi Kulinganishwa | 45 | 43 |

Angalizo: (*) Kutokana na idadi ndogo ya shule za binafsi, ni shule za umma pekee ndio zimejumuishwa katika duru la pili vile vile (**) Takwimu za Nigeria ni wastani wa majimbo 4 yaliyofanyiwa utafiti, ambayo ni Anambra, Bauchi, Ekiti, na Niger. (+) Nchini Msumbiji, Senegal, na Tanzania 2011 (awamu ya 1) ni shule za umma pekee zilifanyiwa utafiti. (+*) Alama hizi za majaribioi ni za wanafunzi waliojaribiwa katika Kiingereza; kwa wale waliojaribiwa katika Kiswahili walipata alama 76.2 katika mtihani uliojumuisha majaribio yote na 80.9 kwenye Kiswahili.

**JEDWALI 3. Kulinganisha matokeo ya SDI kwa Eneo la Kijiografia**

| | TANZANIA 2014 | Tanzania 2010 | Kenya 2012 | Msumbiji | Nigeria* | Togo | Uganda |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Alama za Jumla (lugha, hesabu, na ufundishaji ) | 48 | Hakuna Takwimu | 58 | 29 | 38 | 35 | 44 |
| | | | ***Kiingereza*** | | | | |
| Wastani wa Alama za Lugha | 42 | 57 | 63 | 34 | 49 | 50 | 54 |
| Zoezi la sarufi | 73 | 73 | 92 | 83 | 64 | 74 | 89 |
| Zoezi la kujaza maneno yanayofaa | 53 | Hakuna Takwimu | 66 | 35 | 38 | 30 | 59 |
| Zoezi la insha | 22 | Hakuna Takwimu | 49 | 10 | 24 | 26 | 37 |
| | | | ***Hesabu*** | | | | |
| Wastani wa Alama za Hesabu | 65 | 63 | 77 | 33 | 42 | 33 | 58 |
| Kujumlisha desimali | 64 | Hakuna Takwimu | 75 | 35 | 34 | 36 | 54 |
| Kulinganisha visehemu | 50 | Hakuna Takwimu | 40 | 17 | 16 | 13 | 21 |
| Kutafsiri Data kwenye Grafu | 27 | Hakuna Takwimu | 60 | 13 | 20 | 14 | 27 |
| Kutoa namba za desimali | 67 | Hakuna Takwimu | 83 | 39 | 45 | 18 | 57 |
| | | | ***Ufundishaji*** | | | | |
| Wastani wa Alama za Ufundishaji | 36 | Hakuna Takwimu | 35 | 15 | 18 | 19 | 25 |
| Kutayarisha mpango wa somo | 58 | Hakuna Takwimu | 39 | 19 | 20 | 27 | 31 |
| Kupima uwezo wa watoto | 18 | Hakuna Takwimu | 33 | 14 | 23 | 33 | 25 |
| Kutathmini maendeleo ya wanafunzi | 22 | Hakuna Takwimu | 29 | 7 | 6 | 6 | 11 |
| Idadi ya waliochunguzwa | 2150 | Hakuna Takwimu | 494 | 673 | 1490 | 631 | 1466 |

Angalizo: *Majimbo yaliyofanyiwa utafiti nchini Nigeria yalikuwa: Anambra, Bauchi, Ekiti, na Niger.

## Kiambatisho. Ufafanuzi wa Viashiria vya Utoaji Huduma katika Elimu

**Kiwango cha utoro shuleni**

Sehemu ya walimu wasiozidi kumi waliochaguliwa kwa kubahatisha ambao hawakuwa shuleni wakati wa ziara ya kushtukiza

**Kiwango cha utoro wa darasani**

Sehemu ya walimu ambao hawakuwa darasani wakati wa masaa yaliyopangwa ya kufundisha kama ilivyoonekana wakati wa ziara ya kushtukiza. Walimu wanaweza kukutwa wakifundisha nje, na hii itahesabika kwamba wapo kazini, kwa madhumuni ya kiashiria hiki.

**Muda unaotumika kufundisha kwa siku (pia hujulikana kama Muda wa Kazi)**

Kiasi cha muda anaotumia mwalimu kufundisha wakati wa siku ya shule. Kiashiria hiki hujumuisha data kutoka kwenye Daftari la Mahudhurio ya Wafanyakazi (linatumika kupima viwango vya utoro), sehemu ya utafiti inayochunguza mwalimu anachokifanya akiwa darasani, na masaa yaliyoripotiwa ya kufundisha. Wakati mwalimu yupo darasani, utafiti unatofautishwa kati ya shughuli za ufundishaji na shughuli zisizo za ufundishaji. Kufundisha kunafafanuliwa kwa upana, na hujumuisha mwalimu anavyojishughulisha na wanafunzi, kusahihisha na kupanga madaraja ya kazi za mwanafunzi, kuuliza maswali, kutahini, kutumia ubao au kuwasimamia wanafunzi wakifanyia kazi mahususi, mazoezi au kuweka kumbukumbu.

**Kiwango cha chini cha maarifa miongoni mwa walimu**

Kiashiria hiki hupima maarifa ya mwalimu na inatokana na majaribio ya hesabu na lugha ambayo yanahusisha mtaala wa shule za msingi na hufanywa na walimu wote wa hesabu au lugha ambao walifundisha darasa la tatu mwaka uliopita, au darasa la nne katika mwaka ambao utafiti umefanyika. Hukokotolewa kama asilimia ya walimu waliopata alama zaidi ya 80% katika jaribio la lugha na hesabu. Alama za mtihani: Kiashiria hiki hupima maarifa ya mwalimu na hukokotolewa kama alama za jumla za jaribio la hesabu, lugha na ufundishaji ambayo huhusisha mtaala wa shule za msingi ambayo hufanywa katika ngazi ya shule kwa walimu wote wa hesabu na lugha ambao walifundisha darasa la tatu mwaka uliopita au darasa la nne katika mwaka utafiti umefanyika.

**Upatikanaji wa Miundombinu**

Wastani halisi wa idadi ya shule zenye miundombinu ifuatayo: umeme unaofanya kazi na usafi wa mazingira.
Na hasa: (i) vyoo vinavyofanya kazi na ambavyo vinaonekana kuwa ni safi, vina faragha na hufikika; na (ii) mwanga wa kutosha kuweza kusoma ubaoni kutoka kona ya mwisho ya darasa.

**Upatikanaji wa vifaa vya kufundishia**

Wastani halisi wa idadi ya shule zilizo na vifaa vifuatavyo: ubao unaofanya kazi pamoja na chaki, penseli, na madaftari. Na hasa: (i) ubao unaofanya kazi na chaki, (ii) mgawanyo wa wanafunzi wenye kalamu ni sawa au zaidi ya 90%, na (iii) mgawanyo wa wanafunzi wenye madaftari kwenye darasa ni sawa au zaidi ya 90%.

**Mgawanyo wa wanafunzi wenye vitabu vya kiada**

Idadi ya vitabu vya hesabu na lugha vinavyotumika na darasa la nne lililochaguliwa kwa kubahatisha ukigawanya na idadi ya wanafunzi waliopo kwenye darasa.

**Uwiano wa mwanafunzi – mwalimu**

Wastani wa idadi ya wanafunzi wa darasa la nne kwa mwalimu wa darasa la nne.
Kiashiria cha upatikanaji wa walimu kinapimwa kama idadi ya wanafunzi kwa mwalimu katika darasa la nne lililochaguliwa kwa kubahatisha katika shule kulingana na daftari la mahudhurio ya darasani.

## *Kuhusu tafiti za Viashiria vya Utoaji Huduma (SDI)*

Utafiti wa Viashiria vya Utoaji wa Huduma (SDI) ulifanyika kati ya mwezi Mei na Septemba 2014. Ukusanyaji wa takwimu ulihusisha shule za msingi 400, walimu 3,692 waliohusika kutathmini utoro, walimu 2,196 kwa ajili ya tathmini ya maarifa, na wanafunzi 4,041 waliofanya mtihani. Matokeo yanatoa picha wakilishi ya ubora wa utoaji huduma na mazingira halisia ambayo ndani yake huduma hutolewa katika mfumo wa huduma ya elimu nchini Tanzania. Utafiti unatoa habari kuhusu maeneo matatu ya utoaji huduma: vipimo vya (i) juhudi za mtoa huduma; (ii) maarifa na uwezo wa mtoa huduma; na (iii) na upatikanaji wa vifaa muhimu, kama vile mizani, vifaa vya msingi na miundombinu (kama vile upatikanaji wa maji safi, umeme, nk.). Tanzania ilikuwa nchi mwanzilishi wa SDI mwaka 2010 na nchi ya kwanza kutekeleza ufuatiliaji wa SDI hivyo kuruhusu mchanganuo wa mwenendo katika utoaji huduma. Tafiti za SDI zinapanuka kwa kasi na zimeshatekelezwa katika nchi nane: Kenya, Msumbiji, Niger, Nigeria, Senegal, Tanzania, Togo, na Uganda. Hii inaruhusu mlinganisho baina ya nchi mbalimbali na kupima utendaji wa nchi.

## *Programu ya Viashiria vya Utoaji Huduma (SDI)*

Programu ya SDI ni ubia wa Benki ya Dunia, Muungano wa Utafiti wa Kiuchumi Afrika (AERC), na Benki ya Maendeleo ya Afrika, ambao unatayarisha na kutaasisisha ukusanyaji wa seti za viashiria ambavyo vitapima ubora wa utoaji wa huduma ndani na miongoni mwa nchi kwa kipindi husika. Lengo kuu ni kuongeza kwa kiwango kikubwa uwajibikaji wa utoaji huduma kote barani Afrika, kwa kutoa zana muhimu za utetezi kwa wananchi, serikali, pia na wafadhili; kufanya kazi kufikia shabaha ya kupata maboresho ya haraka katika uitikiaji na ufanisi wa utoaji huduma.

Habari zaidi kuhusu zana za utafiti na data za SDI, na habari za jumla kuhusu programu ya SDI zinaweza kupatikana katika tovuti: www.SDIndicators.org na www.worldbank.org/SDI, au kwa kuwasiliana na barua pepe: SDI@worldbank.org.

© 2016 International Bank for Reconstruction and Development / Benki ya Dunia 1818 H Street NW

Washington DC 20433

Simu: +1 202-473-1000 Tovuti: www.worldbankgroup.org

Kazi hii ni matokeo ya programu ya Viashiria vya Utoaji Huduma (SDI) (www.SDIndicators.org, www.worldbank.org/SDI) na wafanyakazi wa Benki ya Kimataifa ya Ujenzi na Maendeleo/Benki ya Dunia. Matokeo, tafsiri na hitimisho zilizoelezwa katika kazi hii sio lazima ziakisi maoni ya Benki ya Dunia, Bodi yake ya Wakurugenzi Watendaji, au serikali wanazowakilisha.

Benki ya Dunia haitoi dhamana kwa usahihi wa data zilizojumuishwa kwenye kazi hii. Mipaka, rangi, viwango au habari nyingine iliyoonyeshwa kwenye ramani yoyote kwenye kazi hii haimaanishi hukumu yoyote kwa upande wa Benki ya Dunia kuhusu hadhi ya kisheria ya nchi yoyote au kuhalalisha au kukubali mipaka hiyo.

Haki na Ruhusa

Maudhui ya kazi hii yanaamuliwa na hakimiliki. Kwa sababu Benki ya Dunia inahimiza utawanyaji wa maarifa yake, kazi hii inaweza kurudufiwa, yote au sehemu yake, kwa madhumuni yasiyo ya kibiashara ili mradi unakiri kwa ukamilifu chanzo cha kazi hii.

Hoja zozote kuhusu haki na leseni, pamoja na haki za ziada zitumwe kwa Ofisi ya Mchapishaji, Benki ya Dunia, 1818 H Street NW, Washington, DC 20433, USA; Nukushi: +1 202-522-2422; barua pepe: pubrights@worldbank.org au sdi@worldbank.org

WORLD BANK GROUP

AFRICAN ECONOMIC RESEARCH CONSORTIUM
Consortium pour la Recherche Economique en Afrique